FUNZO LA 16

1. Je, Kaini na kizazi chake waliishia nini maisha yao?
-Waliishia anasa, pesa na mali.

2. Kwa sababu Kaini alimuua Habili, je, hio ilimzuia Mungu kufanya kile alichokuwa amepanga kufanya?
-La.
-Hakuna anayeweza kumzuia Mungu kufanya kile alichopanga kufanaya.

3. Kwa sababu Kaini alimuua Habili, Je, Mungu alisahau ahadi yake ya kumtuma mwokozi?
-La.
-Mungu hasahau ahadi zake.

4. Je, kwa nini Mungu aliwapa Adamu na Hawa mwana mwingine aitwae Sethi?
-Kwa sababu Kaini alimuua Habili, Mungu aliamua kutuma mwokozi kupitia kizazi cha Sethi.

5. Kwa nini Adamu alikufa?
-Kwa sababu Adamu hakumtii Mungu, na alimsikiliza Shetani.

6. Kwa nini watu wote hufa?
-Kwa sababu ya dhambi zetu.

7. Je, adhabu ya Mungu kwa dhambi ni nini?
-Kifo.



8. Je, Henoko alijua nini kujihusu?
-Henoko alijua kuwa alikuwa mzaliwa wa Adamu na Hawa.
-Henoko alijua kuwa alizaliwa nje ya Bustani ya Edeni.
-Henoko alijua kuwa alizaliwa katika dhambi.
-Henoko alijua kuwa alizaliwa katika kifo.

9. Je, Henoko alijua nini kumhusu Mungu?
-Henoko alijua kuwa Mungu ni mtakatifu.
-Henoko alijua kuwa Mungu huadhibu dhambi zote kwa kifo.
-Henoko alijua kuwa ni Mungu pekee angeweza kumuokoa.
-Henoko alijua kuwa Mungu angemtuma mwokozi kuwaokoa watu kutoka kwa Shetani.

10. Ni nini cha kushangaza kilichomfanyikia Henoko?
-Mungu alimchukuwa Henoko Mbinguni kwenda kuwa na Mungu.

11. Je, mbinguni kunakaa vipi?
-Mbinguni ni mahali pazuri, ambapo hakuna huzuni wala machozi, ambapo hakuna magonjwa au kifo.

12. Je, kwa nini Mungu alimchukuwa Henoko kwenda mbinguni?
-Kwa sababu Henoko alimtii Mungu.
-Kwa sababu Henoko alimwendea Mungu kwa njia ya Mungu pekee.

-Baada ya Mungu kumchukuwa Henoko, miaka mingi ilipita, na watu wengi wakazaliwa duniani.

-Ijapokuwa kizazi cha Sethi na Henoko kiliendelea kumfuata Mungu, watu wengi waliendelea kumsikiliza Shetani.

Tusome Mwanzo 6:1-2

1-Ikawa wanadamu walipoanza kuzidi usoni pa nchi na wana wa kike walizaliwa kwao,
2-wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wote waliowachagua.

-Je, wana wa Mungu ni nani?

-Walikuwa ni kizazi cha Sethi.
-Walikuwa watu walioamini Mungu.

-Je, binti wa binadamu ni nani?

-Walikuwa binti wa uzao wa Kaini.

-Walikuwa ni wanawake wasiomwamini Mungu.

-Je, wana wa kizazi cha Sethi waliwafanyia nini binti wa uzao wa Kaini?

-Wana wa kizazi cha Seti walianza kuoa binti wa kizazi cha Kaini.

-Watu waliomwamini Mungu wakaanza kuoa wanawake wasiomwamini Mungu.



-Je, nini kilichofanyika wakati wana wa kizazi cha Sethi kilipooa binti wa kizazi cha Kaini?

-Watu wengi zaidi hawakutaka kumsikiliza Mungu.
-Watu wengi zaidi walimsikiliza Shetani pekee.

-Watu wengi zaidi hawakufuata njia ya Mungu.
-Watu wengi zaidi walifuata njia zao wenyewe.

-Je, unafikiri kuwa Mungu alifurahia kuwa watu wengi zaidi hawakutaka kumsikiliza yeye?

Tusome Mwanzo 6:3

3-Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa sababu yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini.

-Mungu hakufurahi kuwa watu wengi zaidi hawakutaka kumsikiliza yeye.

-Je, kwa nini Mungu alitaka watu wamsikilize?
-Ili hao watu wasiharibiwe.

-Mungu alisema kuwa angenena na hao watu kwa miaka 120 pekee.

-Je, kama hao watu wangekataa kumsikiliza Mungu, Mungu angefanya nini?

-Mungu angewaadhibu wote kwa kifo.

-Je, Mungu alikuwa akinena vipi na watu?

-Mungu Roho Mtakatifu alikuwa akinena na hao watu katika akili zao.

-Je, Roho Mtakatifu alikuwa akiwaambia nini watu?

-Mungu Roho Mtakatifu alikuwa akiwaambia watu wamsikilize Mungu wala sio Shetani.

-Mungu Roho Mtakatifu pia alikuwa akiwaambia watu wafuate njia ya Mungu wala sio njia zao wenyewe.

-Je, Shetani hunena na watu kwa akili zao?
-Ndiyo.

-Je, Shetani anawaambia nini watu?

-Shetani anawaambia watu wasimsikilize Mungu.

-Je, kwa nini Shetani hataki watu wamsikilize Mungu?

-Shetani hataki watu wamsikilize Mungu ili waharibiwe.

-Ukikataa kumsikiliza Mungu akinena na wewe katika akili yako, Mungu atakuwadhibu.

-Je, si ni bora kumsikiliza Mungu kuliko kumsikiliza Shetani?



-Hata kama Mungu Roho Mtakatifu alizungumza na watu, je, watu walimsikiliza Mungu?

Tusome Mwanzo 6:11

11-Dunia ikaharibika mbele za Mungu, dunia ikajaa dhuluma.

-Hata kama Mungu Roho Mtakatifu alizungumza na watu, watu wengi walikataa kumsikiliza Mungu.

-Na dunia ikajaa dhuluma.

-Je, watu wa wakati wa Nuhu walikuwaje?

-Walikuwa wabinafsi.
-Walikuwa walafi.

-Walikuwa na wivu kwa wenzao.
-Waliwalaghai watu wengine.

-Waliwadanganya wenzao.
-Waliongea maovu kuhusu wenzao.
-Walichukia wenzao.

-Walikuwa waovu.
-Walikuwa wenye dhuluma.

-Walipigana na wenzao.
-Waliua watu wengi.

-Hawakutaka njia ya Mungu.
-Walitaka tu njia yao.

-Je, watu wa sasa wako kama watu wa wakati wa Nuhu?
-Ndiyo.

-Je, watu wa sasa ni wachoyo na walafi?
-Ndiyo.

-Je, watu wa sasa huongea uovu na kuwadanganya wenzao?
-Ndiyo.

-Je, watu wa sasa hupigana na wenzao na kuwaua?
-Ndiyo.

-Je, watu wa sasa hutaka njia yao ila si ya Mungu?
-Ndiyo.

-Hao watu walizaliwa wenye dhambi kwa sababu ni kizazi cha Adamu na Hawa.

-Watu wa sasa pia wamezaliwa wenye dhambi kwa sababu ni kizazi cha Adamu na Hawa.

-Watu wote wamezaliwa wenye dhambi kwa sababu ni kizazi cha Adamu na Hawa.

-Je, Mungu aliona dhambi za watu?

Tusome Mwanzo 6:5 & 12



5-Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote.
12-Mungu akaiona dunia, na tazama, imeharibika; maana kila mwenye mwili amejiharibia njia yake duniani.

-Je, Mungu aliona dhambi za watu?
-Ndiyo, Mungu aliona dhambi zao zote.

-Mungu huona kila dhambi.

-Hakuna anayeweza kuficha dhambi yeyote kwa Mungu, kwa sababu Mungu yuko kila mahali.

-Mungu huona kila dhambi, na anaadhibu kila dhambi.

-Mungu huona kila dhambi, na anaadhibu kila dhambi kwa kifo.

-Je, Mungu alifikiria nini alipoona watu wote wakitenda dhambi?

Tusome Mwanzo 6:6-7

6-Bwana akaghairi kwa sababu amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo.
7-Bwana akasema, Nitamfutilia mbali mwanadamu niliyemuumba usoni pa nchi; mwanadamu na mnyama, na kitambaacho na ndege wa angani; kwa maana naghairi ya

kwamba nimewafanya.

-Mungu alihuzunishwa sana na dhambi za watu wote.

-Je, Mungu aliamua kufanya nini kwa sababu dunia ilijawa na dhambi za watu wote?

-Mungu aliamua kuwaharibu watu wote duniani.

-Kwa sababu dunia ilijawa na dhambi za watu, Mungu aliamua kuharibu vyote vyenye uhai duniani.

-Je, unafikiri kuwa Mungu alizungumza tu?

-Ama unafikiri kuwa Mungu angefanya kile alisema atafanya?

-Mungu aliwaambia Adamu na Hawa wangekufa na kutengana na yeye kama wangekula lile tunda alilowakataza.

-Je, Mungu alizungumza tu, au Mungu alifanya alichosema atafanya?

-Mungu alifanya alichosema atafanya.

-Mungu aliwaambia Kaini na Habili kuwa lazima waje kwa Mungu kupitia njia ya Mungu au wangekataliwa.

-Je, Mungu alizungumza tu, au Mungu alifanya alichosema atafanya?



-Mungu alifanya alichosema atafanya.
-Mungu si kama watu.

-Watu husema watafanya jambo, lakini hawalifanyi.

-Ila Mungu si kama watu.

-Mungu kila wakati hufanya kile alisema atafanya.

-Kwa sababu ya upendo na huruma za Mungu, kulikuwa na mtu mmoja ambaye Mungu hangemwangamiza.

Tusome Mwanzo 6:8-10

8-Lakini Nuhu akapata neema machoni pa Bwana.
9-Hivi ndivyo vizazi vya Nuhu. Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Nuhu alikwenda pamoja na Mungu.
10-Nuhu akazaa wana watatu wa kiume, Shemu, na Hamu, na Yafethi.

-Je, kwa nini Mungu aliamua kumuhifadhi Nuhu?

-Je, ni kwa sababu Nuhu hakuwa ametenda dhambi?
-La.

-Nuhu alikuwa amezaliwa katika dhambi kama watu wote.

-Nuhu alizaliwa mtumwa wa shetani kama watu wote.

-Je, kwa nini Mungu aliamua kumuhifadhi Nuhu?

-Kwa sababu Nuhu hakumsikiliza Shetani.
-Kwa sababu Nuhu alimsikiliza Mungu.

-Kwa sababu Nuhu hakufuata njia yake mwenyewe.
-Kwa sababu Nuhu alifuata njia ya Mungu pekee.

-Kwa sababu Nuhu alijua kuwa Mungu angetuma Mwokozi.

-Je, kwa nini Mungu aliamua kumuokoa Nuhu?

-Kwa sababu Nuhu alijua kuwa alizaliwa katika dhambi.
-Kwa sababu Nuhu alijua kuwa alimtendea Mungu dhambi.

-Kwa sababu Nuhu alijua kuwa Mungu huadhibu dhambi zote kwa kifo.

-Kwa sababu Nuhu alijua kuwa ni Mungu pekee aliyeweza kumuokoa.

-Kwa sababu Nuhu alijua kuwa Mungu angemtuma mwokozi wa kumuokoa katika dhambi.

-Kutokana na Neema ya Mungu, Mungu aliamua kumuhifadhi Nuhu.

-Neema ni nini?

-Ufuatao ni mfano:



-Mwizi alimuibia jirani yake mara nyingi.

-Siku moja, huyo mwizi akanaswa katika mafuriko ya mto.

-Huyo mwizi alikuwa akizama katika huo mto.

-Lakini jirani yake, alimuona huyo mwizi, akamvuta kutoka mtoni, akamuokoa.

-Ingawa huyo mwizi alikuwa ameiba mara nyingi, jirani yake alimuokoa.

-Ingawa huyo mwizi alistahili kuzama, jirani yake alimuokoa.

-Hio ni neema.

-Hivi ndivyo Mungu hutuokoa tunapomwamini yeye pekee.

-Kwa sababu Nuhu alimwamini Mungu, na Mungu akaamua kumwokoa Nuhu, Mungu alimpa Nuhu amri.

Tusome Mwanzo 6:13-14

13-Mungu akamwambia Nuhu, Mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia.
14-Ujifanyie safina ya mti wa mvinje; fanya na vyumba ndani ya safina, ukaifunike ndani na nje kwa lami.

-Je, Mungu alimwamuru Nuhu kufanya nini?

-Mungu alimwamuru Nuhu kujenga safina.

-Je, kwa nini Mungu alimwamuru Nuhu kujenga safina?

-Kwa sababu Mungu alipanga kutuma gharika kuharibu uhai wote duniani.

-Mungu alimpa Nuhu amri nyingi kuhusu jinsi ya kutengeneza hio safina.

Tusome Mwanzo 6:15-21

15-Hivi ndivyo utakavyoifanya; mikono mia tatu urefu wa safina, mikono hamsini upana wake, na mikono thelathini kwenda juu kwake.
16-Uifanyie safina mwangaza, ukaumalize juu kiasi cha mkono mmoja; ukautie mlango wa safina katika ubavu wake; ukaifanyie dari tatu, ya chini, ya pili, na ya tatu.
17-Na tazama, nitaleta gharika ya maji juu ya nchi, niharibu kila kitu chenye mwili na pumzi ya uhai, kisiwepo chini ya mbingu; kila kilichoko duniani kitakufa.
18-Lakini nitafanya agano langu nawe kuwa thabiti; nawe utaingia katika safina, wewe, na wanao, na mkeo, na wake za wanao, pamoja nawe.
19-Na katika kila kilicho hai chenye mwili, wawili wa kila namna utawaleta ndani ya safina, kuwahifadhi pamoja nawe; wawe mume na mke.
20-Katika vyote virukavyo kwa jinsi yake, na kila namna ya mnyama kwa jinsi yake, kila kitambaacho juu ya nchi kwa jinsi yake, wawili wa kila namna watakuja kwako ili



uwahifadhi.
21-Ukajitwalie chakula cha kila namna kinacholika, ukakusanye, nacho kitakuwa ni chakula chenu na chao.

-Mungu alimwamuru Nuhu kujenga safina kwa urefu hakika.
-Mungu alimwamuru Nuhu kujenga safina kwa upana hakika.

-Mungu alimwamuru Nuhu kujenga safina kwa kimo hakika.

-Je, Mungu alitaka Nuhu ajenge safina kwa njia ya Nuhu?
-La.

-Mungu hakutaka Nuhu ajenge safina kwa njia ya Nuhu.

-Je, Mungu alitaka Nuhu ajenge aje safina?
-Kama vile Mungu alivyoamuru.

-Mungu alimtaka Nuhu ajenge safina kama vile Mungu alivyotaka.

-Mungu alimtaka Nuhu ajenge safina kwa njia ya Mungu pekee.

-Mavazi ya Adamu na Hawa yalitengenezwa kwa njia ya Mungu pekee.

-Dhabihu ya Kaini na Habili ilipaswa kuwa kwa njia ya Mungu pekee.

-Safina ya Nuhu ilipaswa kujengwa katika njia ya Mungu

pekee.

-Je, Mungu alimwamuru Nuhu kujenga safina ngapi?
-Moja tu.

-Kulikuwa na safina moja tu ambayo ingemuokoa Nuhu.
-Hakukuwa na safina nyingine ambayo ingemuokoa Nuhu.

-Je, Mungu alimwamuru Nuhu kujenga milango mingapi katika mashua?
-Mmoja tu.

-Kulikuwa na mlango mmoja tu ambao Nuhu angeingilia ili aokolewe.

-Hakukuwa na mlango mwingine ambao Nuhu angeingilia ili aokolewe.

-Je, unafikiri kuwa Nuhu alimtii Mungu?

Tusome Mwanzo 6:22

22-Ndivyo alivyofanya Nuhu, sawasawa na vyote alivyomwamuru Mungu, hivyo ndivyo alivyofanya.

-Nuhu alimwamini Mungu.
-Nuhu aliamini kuwa Mungu hadanganyi.

-Nuhu aliamini kuwa Mungu angetuma gharika kama vile alivyosema atafanya.



-Kwa hivyo, Nuhu akajenga mashua kama alivyosema Mungu.

-Ingawaje Nuhu hakuwa amewai kuona mvua awali, Nuhu aliamini nini?

-Kuwa Mungu angetuma gharika.

-Ingawaje hakuna aliyekuwa ameona mvua awali, Nuhu aliamini nini?

-Ya kuwa Mungu angetuma gharika.

-Je, Nuhu alifanya nini alipokuwa akijenga safina?

-Nuhu alipokuwa akijenga safina, aliwaambia watu wamsikilize Mungu.

-Nuhu alipokuwa akijenga safina, aliwaambia watu wamwamini Mungu.

-Nuhu alipokuwa akijenga safina, aliwaambia watu kuwa Mungu angetuma gharika ili kuiharibu dunia.

-Kama vile nakuwambia kumhusu Nuhu, hivyo pia ndivyo Nuhu aliwaambia watu kumhusu Mungu.

-Je, unafikiri kuwa watu walimsikiliza Nuhu?

-Tutajua katika funzo lifuatalo.